


Unachotakiwa kujua kuhusu udhibiti wa Ndigana kali

Ndigana kali ni ugonjwa hatari wa ng'ombe unaoenezwa na kupe wekundu wanaokaa katika masikio ya ng'ombe. Ugonjwa huu unasababisha vifo na hasara kubwa kiuchumi.




Dalili za ugonjwa

- Joto kali, centigrade 40 au zaidi
- Machozi kutiririka machoni
- Kuvimba tezi
- Kuhema kwa taabu haraka haraka
- Kuto kwa mate na kukohoa katika hatua za mwisho
- macho kuonekana meupe
- Kupungua uzito haraka

Namna ya kuzuia ndigana kali

- Chanjo hii inayotolewa mara moja katika maisha yote ya ng'ombe ni njia madhubuti ya kudhibiti Ndigana kali.



Unachotakiwa kuzingatia wakati wa kuchaanja

- Chanjo itolewe na mchanjaji aliyesajiliwa. wasiliana na mwagizaji wa chanjo aliye karibu ili kupata huduma ya mchanjaji
- Jadiliana na mchanjaji ili kujua siku ya kukusanya wanyama watakaaochanjwa
- Kuchanja ndama kunapunguza gharama na kuleta tija
- Ng'ombe aliyechanjwa awekewe hereni sikioni ya kumtambulisha
- Mnyama aliyechanjwa atapewa dawa ya minyoo

Faida za chanjo ya Ndigana kali

- Udhibiti wa kupe kwa kuogesha katika joshu au bomba la mkono ni ghali
- Uogeshaji kwa ng'ombe aliyechanjwa unapungua na hivyo kuokoa fedha
- Gharama ya kutibu ugonjwa huu hatari inaepukwa
- Chanjo inatolewa mara moja katika maisha yote ya ng'ombe
- Chanjo ya Ndigana kali inamuwezesha mfugaji kufuga ng'ombe wa kisasa wenye uzalishaji mkubwa



Waagizaji wa chanjo ya Ndigana kali waliothibitishwa na Serikali ya Tanzania

- Dr. Nderingo Ngowi, Pharmavacs Limited: Telephone: +255(0)784918504
- Dr. Lwitiko Saidi Mwakalukwa, Vetlife consultants Limited, Mbeya: Telephone: +255(0)767346793
- Dr. Henry Mbwille, Ronheam International Company limited: Telephone: +255(0)755327016
- Dr. Charles Dulle, Dulle Veterinary centre: Telephone: +255(0)754632648